# Kwa Nini Kiswahili Kinazungumzwa Kusini mwa Somalia

*V. Nkondokaya*

## 1.0 Utangulizi

Makala haya yanajaribu kueleza historia ya watu wanaozungumza Kiswahili huko Somalia ambao si Wasomali kwa asili. Katika kueleza historia ya watu hawa tutaonyesha jinsi Kiswahili kilivyoenea kutoka Afrika Mashariki hadi kufika huko Somalia ya Kusini.

Kwa mujibu wa Mbitta (1966) watu wanaozungumza Kiswahili huko Somalia Kusini ni Wazigua waliohamia huko miaka mingi ilyopita. Wazigua hawa wanaishi katika wilaya ya Chamama, moja ya wilaya nne za mkoa wa Juba ambao hujulika kwa Kisomali kama Jubadda Hoose (Juba ya Kusini) na mji wake mkuu ni Kisimayu. Wilaya nyingine za mkoa wa Juba ni Badada, Kismayu na Afamadow. Mkoa wa Juba wenye kupakana na Kenya. Una wakazi wengine mbali na Wazigua ambao pia wana asili ya Kibantu.

## 2.0 Historia ya Wazigua wa Somalia

Wazigua wa Somalia asili yao ni Handeni na waliondoka huko yapata miaka 550 – 600 iliyopita. Baba wa Taifa Mwalimu J.K. Nyerere alipata nafasi ya kuwatembelea huko Somalia mwaka 1966 (taz. Nchi Yetu tol. 33,1966) wakati alipofanya ziara ya kiserikali huko Somalia.

Historia ya Wazigua inahusishwa na Wanguu, Wasambaa, Wabondei, Wakilindi, na Waluvu ambao kwa pamoja wanajumuishwa katika historia ya Waseuta. Kutokana na sababu za kihistoria na kijiografia Wazigua wanapakana na makabila ya pwani ya Afrika Mashariki kulipochipukia Kiswahili. Kutokana na mazingira haya Wazigua wana umilisi mkubwa wa Kiswahili. Japokuwa asili ya Wazigua ni Handeni ambayo yajulikana kama Zigua Kuu au Zigua la Kwanza, kwa sasa wametapakaa Pangani na Korogwe katika mkoa wa Tanga, Saadani, Bagamoyo, Kibindu Kwa Malungo, Mbwewe, Miono, Msata, Lugoba n.k. katika mkoa wa Pwani na Morogoro Vijijini katika mkoa wa Morogoro.

## 3.0 Kuhama kwa Wazigua na Kwenda Somalia

Kuhama kwa baadhi ya Wazigua na kwenda Somalia na kushindwa kurejea tena Zigua, kulitokana na sababu za kiuchumi na kijiografia. Kutokana na njaa kubwa iliyotokea Uzigua miaka 550–600 iliyopita kikundi cha Wazigua kiliondoka na Wasomali waliokuwa wakiishi Uziguani na kwenda Somalia katika nchi za Barawa na Merka ambapo kulikuwa na chakula kwa wingi. Njaa hiyo ilijulikana kama "Gumbo dya Kidyanchingo" yaani 'njaa ya kula ngozi' au 'njaa ya ngozi' (taz. Mbitta 1966, Simba 1932 na Mochiwa 1972). Walisafiri

kwa majahazi hadi Barawa pamoja na Wabarawa wenyeji wa huko Somalia, na Waarabu. Baada ya miaka miwili walitamani kurejea kwao lakini wenyeji wao wakakataa kuwarejesha na kuwaambia kuwa walikuwa watumwa wao. Wazigua walikataa kuwa watumwa na kuamua kuondoka Barawa na Merka kwa miguu kurejea kwao wakiambaa pwani ya bahari ya Hindi kwa matarajio kuwa wangefanikiwa kufika Tanga wakifuata machweo ya jua kwa vile upande wa kusini kuelekea Tanga ndio machweo ya jua kwa Somalia. Katika safari hii walipita msituni na kupambana na wanyama wakali. Hatimaye walifika eneo la mto Juba lenye ardhi nzuri ambalo walilipenda na kujenga miji yao na kuishi. Baada ya miaka mingi kupita waliamua kutoendelea na safari ya kurudi kwao na badala yake kupanua himaya yao hadi pwani ya Kisimayu. Pamoja na kuishi katika nchi hii ya kigeni hawakusahau mila, tabia na desturi za kwao na hata majina ya nchi, miji na vijiji na hata ya watu waliyaendeleza huko mpaka leo. Sasa na tutazame baadhi ya sababu zilizofanya Kiswahili kuzungumzwa katika eneo hilo la kusini mwa Somalia.

## 4.0 Kuenea kwa Kiswahili Somalia

Kiswahili kilienea hadi Somalia kwa njia kadhaa, hapa tutataja tatu:

1. *Wazigua waliohamia Somalia walikieneza huko.*

Wazigua waliposafirishwa hadi eneo la Barawa walikwenda wakiwa Waswahili kamili kwani walitoka maeneo kama Handeni, Pangani, Saadani na Bagamoyo ambapo Kiswahili kimekuwa kikizungumzwa. Hivyo mbali ya Kizigua pia walikuwa wanaongea Kiswahili, walipofika Somalia walikipandikiza huko Barawa na baadaye katika eneo la Kusini zaidi yaani eneo la Juba na Kismayu walikohamia baadaye. Hivyo basi kuwepo kwao sehemu hii ya Somalia kumesaidia Kiswahili kuzungumzwa sana.

2. *Kiswahili kilienezwa Somalia na Wasomali wa Barawa*

Wabarawa walikuwa na mazoea ya kuja pwani ya Afrika Mashariki ambapo walijifunza Kiswahili ili kurahisisha mawasiliano na wenyeji katika shughuli zao za biashara. Kwa hivyo waliporejea kwao Barawa waliendelea kukizungumza huko. Walikuja huku wakisafiria majahazi na ushahidi wa kuja kwao huku ni makaburi yao yaliyopo hadi leo eneo la Kunduchi Dar es Salaam (taz. Chiraghdin na Mnyampala: 1977).

3. *Ujirani na pwani ya Kenya*

Sababu nyingine ya tatu ni eneo hili la Somalia Kusini kuwa karibu na maeneo ya Kenya kama Lamu, Faza, Siu, Pate, Manda, Malindi n.k. ambako Kiswahili kinazungumzwa sana. Hivyo kwa kuwa karibu, ni wazi yalikuwapo mawasiliano mengi kati ya watu wa maeneo haya yaliyotenganishwa na mpaka tu.

Wazigua wa Somalia wanaweza pia kuongea Kisomali, Kiarabu, Kitaliano na Kiingereza kwa vile eneo la kusini lilikuwa chini ya Wataliano toka Vita Kuu ya Kwanza ya dunia na lile la kaskazini chini ya Uingereza. Hata hivyo miaka 12 kabla ya Uhuru wa Somalia hapo mwaka 1960, Umoja wa Mataifa uliikabidhi rasmi Italia kuisimamia na kuiandaa Somalia kwa ajili ya Uhuru wake. Hata njia kuu ya mawasiliano nyakati hizo kwenda maeneo ya Lamu na Mombasa kutoka Somalia ilikuwa sharti ipitie Kismayu.

**4.1 Ushahidi wa Kiswahili kuzungumzwa Somalia**

Mbali na habari za kuwepo kwa Wazigua wanaozungumza Kiswahili huko Barawa ambao walieneza Kiswahili huko, kitabu cha ramani ya lugha za dunia kiitwacho "Atlas of the World's Languages" (Moseley & Asher, 1994 uk. 280 ramani namba 77) nacho kinaonyesha kuwa lugha hii ilizungumzwa huko.

Kitabu hiki cha ramani kinaonyesha nchi mbalimbali duniani na lugha zao na katika uk. 280 kuna ramani ya Somalia na katika maeneo ya Barawa, Juba na Kismayu yamewekewa mzunguko wa rangi ya pinki ambao unaeleza kuwa Kiswahili kinazungumzwa sana katika maeneo hayo. Juba ndilo eneo la Wazigua wa huko Somalia na lile la Barawa ndilo walilofikia Wazigua kwanza.

**5.0 Kudumishwa kwa Majina ya Kizigua huko Somalia**

Majina ya miji na vijiji vya huko Somalia yanaakisi yale ya Uzigua na nchi ya Waswahili kutoka pwani ya Tanga, Pangani hadi Bagamoyo. Majina hayo ni kama Gobweni, Boma ya Chamama, Mlima Mboga, Yonte, Faruwama, Urikui Zunguni, Harara, Pangani, Bagamoyo Sherji, Murjani, Mauya, Borini, Mgambo, Fara, Mofi, Kwa Mofi, Mwana Mofi, Chamama, n.k. Miji mingine ni Kwamswagiro, Kwamwegwa, Kwamwigwa, Kwamachaku, Kwamusa, Songo Dunia n.k. Asili ya majina yote haya, ni miji na vijiji vilivyoko katika tarafa za Mazingara, Mgambo na Kwamsisi (Handeni) na mingine ni maeneo ya Pangani na Bagamoyo. Majina yote yana maana kwa Kizigua.

Tumeona kuwa Wazigua wa Somalia huishi mkoa wa Juba kando ya mto Juba. Eneo wanakoishi Wazigua hawa linaitwa Chamama na linajulikana kama Zigua la Pili na huko hufahamika kwa jina la *Wagosha wa Juba.* Katika mkoa huu yapo pia makabila machache ya Kibantu kama vile Wagobawein, Wahelai, Wa Tunni Torre, Wa Re Issa, Wakabole, Wamakanne pamoja na Wagosha (Wabajuni, Waboni, Waeile na Wa-Amar-anni (ambao nao wanazungumza Kiswahili). Kismayu ni moja kati ya miji mikubwa ya Somalia, miji mingine mikubwa baada ya Mogadishu ni Hargeysa, Berbera na Merca. Kwa vile sehemu kubwa ya Somalia ni jangwa baadhi ya makabila yakiwemo Wagala na Wasomali walijaribu kuwaondoa Wazigua eneo hilo lenye rutuba kwa vile liko kando kando ya mabonde ya mto mkubwa wa Juba, lakini wote walishindwa.

Ni muhimu ifahamike pia kuwa yapo makabila mengine yaliyotoka Tanzania ambayo nayo yalihamia huko. Makabila ambayo yanatajwa kuwa yaliongozwa na Wazigua kutoka Merka na Barawa katika jaribio la kurudi nyumbani Tanzania, japo watu wake walikuwa wachache. Makabila hayo ni Wayao, Wazaramo, Wangindo, Wamakuwa, Wasukuma, Wanyamwezi, Wadoe, Wakwere na kutoka Kenya ni Wapokomo, Wakamba, Wakalanje na wengine.

Baada ya kukwama na kuamua kuishi nchi walipo leo, makabila yote haya yalimezwa na Wazigua na leo hili wanaongea Kizigua na wengi wamepoteza kumbukumbu zao za zamani na kuwatambua si rahisi. Wazigua halisi wa Somalia husema kuwa huwatambua wale wasio Wazigua kwa asili kwa kuchunguza mambo ya kimila hasa harusi, misiba, miviko n.k. ambayo ni tofauti na ya Wazigua. Baadhi ya makabila haya yaliamua kuwa na miji ya peke yao ili wasimezwe na Wazigua. Walijenga miji yao kandokando ya mto Juba toka pwani za Kismayu na Gobweni hadi Gelib.

### 5.1 Tafsiri mbalimbali za miji na vijiji vya Uzigua ya Somalia

Ili tupate tafsiri mbalimbali ya miji hii ya Wazigua na kuielewa, tuanzie pwani ya Kismayu mpaka Komtire. Miji yote ya Wagosha kama tulivyoona imejipanga kulia na kushoto mwa mto Juba. Barabara ya kwenda Uzigua inatokea Kismayu, barabara hii pia ni ile itokayo nchi jirani ya Kenya. Kwa ufupi kutoka Kenya kwa usafiri wa bahari au barabara kwenda Uzigua sharti upite Kismayu. Tafsiri na maana ya majina haya yatazidi kutupa mwanga zaidi wa uhusiano wa nchi hii ya Wazigua na Uswahili wa huku kwetu:

*Kismayu* ni jina la mji ambao unafikiriwa kuitwa hivyo na Wazigua wa huko kutokana na maneno ya Kiswahili "Kisima cha Juu" au "Kisima ya Juu". kwa Kiswahili cha huko Somalia.

*Gobweni* ni jina la mji wa Wazigua wa Somalia ambao unahusishwa na "Bweni" ambalo ni jina la eneo fulani huko Pangani, Tanzania. Inafikiriwa kuwa wakazi wa mji huenda walitokea Pangani Tanzania.

*Mpangeni au Pangeni* ni jina la mji wa Wazigua unaohusishwa na mji wa Pangani ulio pwani ya Tanzania huko Tanga.

*Zunguni* ni mahali alipokuwa anakaa Mzungu yaani "Ko Mzungu" au "Kwa Mzungu".

*Chamama* ni jina la mji mkuu wa wilaya wanakoishi Wazigua huko. Mahali hapa hujulikana pia kama "Bwila" ambayo kwa Kizigua humaanisha "Hapa Tumefika" (hatuondoki tena).

*Mwanamofi* ni jina la mji linalotokana na neno la Kizigua *mofi* ambalo linahusishwa na Wazigua wanaoitwa Wamofi ambao wanaishi Kwamkono katika kijiji cha Kwamnele kinachozunguka kilima kinachoitwa *Kofi* huko Uzigua

*Mbuliyaga* na *Mbulizaga* ina maana ya "Mambo au juhudi au Habari zote zimepotea". Waliposhindwa kurudi Handeni walikata tamaa hivyo wakaanzisha miji na kuipa majina haya – kuonyesha kuwa juhudi zote za kurudi nyumbani zimeshindikana. Pia haya ni majina ya miji huko Pangani.

*Mauya ni* mji uliojengwa na Wazigua waliojaribu kurejea kwao na kushindwa hata kurudi tena Somalia na kuuita mji huo Mauya yaani "Waliorudi". Baada ya jaribio la kurudi nyumbani kushindikana miaka mingi baadaye kundi fulani la Wazigua lilivuka mpaka na kuingia Kenya. Hata hivyo wakiwa Kenya bara ya visiwa vya Lamu waliona hawatafika, wakaamua kurudi tena Somalia wakajenga mji wakauita jina hili. Watu wa sehemu hii huzungumza lugha ya Kizigua hata kupita sehemu zote za Wazigua wa Tanzania na Somalia.

Miji mingine ya Zigua ya Somalia ni kama vile: Kiva (au Chiva), Lomwe, Bagamoyo, Pangani, Komzundu, Kwamwanamwemzundu, Mabungu, Mwembeni, Songo Dunia, Kwa Samuya Ngoto, Fara, Kwa Musa, Kobongo,(au Kabongo), Kwa Luchindo, Sherji, Fikiro, Takaungu, Kwa Samuya, Musa Haji, Mibuyuni, Kwalugulu, Kibindu, Kwamwigwa, Mgambo, Kwamchala, Chikwazu, Mgambo, Mlimamboga, Urikui, Takaungu, Harara, Chigola, Mbolini na miji mingine mingi. Majina yote haya yapo Uzigua ya Handeni katika tarafa za Mgambo, Mazingara na Kwamsisi, na Zigua za Pangani na Bagamoyo. Kuwapo kwa miji hii huko Uzigua ya Somalia kunaonyesha kuwa watu wa miji hii walitoka kwenye miji ya majina hayo hayo iliyopo Tanzania.

*Tanzania* ni jina la kijiji cha Wazigua huko Somalia ambacho wakazi wake walikiita hivyo ili kuashiria kuwa wao wana asili ya Tanzania (si wenyeji wa Somalia).

*Chizumo* ni neneo lenye kumaanisha "kelele kubwa zenye kutikisa nchi", Jina hili lilipewa mahali ambapo Wazigua waliwazomea Wasomali baada ya kuwapiga kwenye vita ya mwaka 1893.

*Hamkwama* ni mahali ambapo Wazigua katika safari ya kurudi waliamua kupumzika (kupiga kambi) na hatimaye walikwama hapo kwani walishindwa kuendelea. Mahali hapo paliitwa mahali walipokwama" au Hamkwama

*Komzuma* (au Kwamzuma) ni mji wa mwisho wa Wazigua ambao kwa sasa wanaishi Wangindo ambao pia wanakaa katika eneo linaloitwa Shongolo Mavula hadi Mkalango.

*Mkalango* ni mji wa Wazigua wenye maana ya mahali ambapo Wasomali walipigwa na 'kukaangwa' (mkalango) kama bisi. Wasomali wanapaita Tolay kwani ni mahali ambapo Wasomali walipigwa mpaka wakalia "Tolay" ikimaanisha "Ukoo uko wapi?" au "tumekosa ukoo" yaani watu wao wanamalizwa na Wazigua.

*Chambike* ni mji uliopewa jina hilo kufuatia jina la kiongozi wa kwanza wa Waseuta aliyeitwa *Chambike Vumba* ambaye alitawala Vumba (katikati ya Mombasa na Tanga). Inadaiwa kuwa neno *chambike* lina asili ya Kiajemi na

kwamba linatokana na jina la mfalme wa Uajemi aliyeitwa 'Cambyses' ambaye alizuru pwani walikoishi Wazigua ambao walimwita *Chambike* katika Kizigua.

*Shongolo mavula* ni jina la mji linatokana na Mzee mashuhuri wa Kingindo ambaye alikuwa akiishi eneo hili. Eneo hili wanaishi leo Wasomali wenye asili ya Kingindo yaani Wangindo wa Somalia.

*Komtire (au Komtile)* ni mji wa Wayao ambao wameenea katika wilaya ya Gelib ambayo ipo katika mkoa Jubadda Dhexe (Upper Juba) huko Somalia. Wazigua na makabila mengine yenye asili ya Tanzania huishi hapa pia. Haya makabila mengine yalifika hapa yakitokea Kisimayu na Gobweni.

*Tumba* ni mji ulio kanda ya mto Juba na jina lake linatokana na eneo lenye jina hili lililoko Handeni Mashariki. Eneo hili linajumuisha tarafa za Handeni za Mgambo, Mazingara, Kwamsisi na Wilaya ya Pangani.

*Gosha* ni mji ambao jina lake linadaiwa kutokana na neno la Kizigua "mgosi" yaani mtu. Inasemekana kuwa Wasomalia walipowasikia Wazigua kila mara wakiitana "mgosi, mgosi" walishindwa kutamka neno hilo hivyo wakawaita "wagosha" hivyo kujulikana kama "Wagosha wa Juba au Wagosi wa Juba" yaani Wagosi au watu wanaoishi Mkoani Juba. Nchi yao na miji yao imejengwa kandokando ya mto Juba toka pwani kwenda kule unakotokea mto, ambao pia huitwa "Mto Gosha"

**6.0 Hitimisho**

Makala haya yameonyesha jinsi Wazigua walivyofika Somalia na kuenea sehemu kadha katika nchi hiyo. Aidha tumeonyesha kuwa mbali ya Wazigua wapo pia Wasomali wengine wenye asili ya Tanzania. Makabila hayo ni kama vile Wayao, Wangindo, Wamakuwa, Wazaramo, Wadoe, Wakwere, Wanyasa na wengine. Makabila haya nayo yalihamia huko kwa sababu mbalimbali hata hivyo watu wa makabila haya hawakwenda wengi kama Wazigua. Kutokana na Mwandishi Daud Deus ambaye ni Mzigua na yupo Mogadishu anataja idadi ya Wazigua huko kuwa kati ya 80 – 110,000. Makabila yote haya yameendelea kurithisha Kiswahili kwa wazao wao hivyo kukifanya kiendelee kudumu huko. Kuwapo kwa makabila haya katika eneo hili la Somalia kunatoa changamoto kwa watafiti wa Kiswahili kufanya utafiti ili kufahamu hali halisi ya Kiswahili huko Somalia.

## Marejeo


Abdalla bin Hemedi' Iajjemy, (962), *Habari za Wakilindi,* DSM: EALB.

Abdallah bin Hemedi Iajjemy, *The Story of Mbega*. TNR 1936 (1937 na. 2&3). Imetafsiriwa toka *Kiswahili na Roland Allen.*

Ali bin Hemed El-Buhiriy, *Habari za Mrima*, DSM : Mambo Leo, 1935-1936.

Chabai, Zakayo (Padre), (1992), *Simo, Njelo na Ngano za Kizigua*, DSM : UNESCO, (kt. 1&2)

Chiraghdin, S. & Mnyampala, M., (1997), *Historia ya Kiswahili.* Nairobi : OUP.

Kilo, Selemani, (1953), *The History of the Zigua Tribe*, DSM: (na. 34) (Imetafsiriwa toka Kiswahili na Petro Sh. Mntambo).

Mbita, Hashim . (1966) *Mwalimu [Nyerere] Awavutia Wasomali*, DSM: Nchi Yetu, Vol. 33 (Safari ya Rais Nyerere huko Somalia).

Mdoe, Bakari, (1935) *Khabari za Wazigua.* DSM: Mambo Leo, Na. 154 & 155.

Mochiwa, Antony (1954), *Habari za Wazigua,* London : EALB & MacMillan.

NCHI YETU, (1966), *Rais Nyerere Atembelea Somalia*, Tol. Na. 33.

SURVEY OF KENYA, (1970), *The National Atlas of Kenya 3rd ed.,* Nairobi: KenyaGovernment, (uk. 85, 97-85).